JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI
AMANI ABEID KARUME
S.L.P. 45,
**KONDOA.**
Tarehe ……………2023.

Namba ya simu:

| | |
|---|---|
| MKUU WA SHULE: | 0785 79 49 80/0735794980 |
| MAKAMU MKUU WA SHULE: | 0714 51 41 47 |
| MWALIMU MALEZI: | 0688 967414 |

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

-----------------------------------------------------------------------
S.L.P. ………………………………………………………………………….
--------------------------------------------------------------

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI AMANI ABEID KARUME HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA, MKOA WA DODOMA MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya ……………… Shule ya Sekondari Amani Abeid Karume ipo umbali wa kilomita 45 Mashariki mwa mji wa Kondoa. Usafiri kutoka mjini Kondoa unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi nauli ni shilingi 3,000/= tu. Utapanda mabasi yaendayo **Busi**, kisha shuka **Pahi**, hapo uliza shule ya Sekondari Amani Abeid Karume. Kwa wale wanaotokea Arusha kupitia Babati utashuka kituo cha **KOLO**, Kilomita 25 kabla ya kufika mjini Kondoa. Uliza magari yaendayo Pahi nauli ni Tsh. 2,000/= kwa basi la abiria na Tsh. 7,000/= kwa usafiri wa bodaboda. Usafiri wa basi upo kila siku kuanzia saa 5:00 asubuhi hadi saa 7:30 mchana.
   Muhula wa masomo Unaanza tarehe 14 Agosti 2023. **Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni Tarehe 14 Agosti 2023**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31 Agosti 2023. mwanafunzi anatakiwa kuwahi kwa ajili ya kuanza masomo.

**2. Mambo Muhimu ya kuzingatia.**

**2:1. Sare ya Shule**

(a) Shati mbili (02) nyeupe mikono mirefu, shati lazima lishonewe alama **V mabegani ikimaanisha namba tano ya kirumi, kitambaa kifanane na rangi ya suruali.** Aje nazo mwenyewe.

(b) Suruali mbili za rangi ya kijivu iliyoiva chini upana inchi 14, aje nazo mwenyewe. Suruali zilizobana haziruhusiwi.
(c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(d) Mwanafunzi anunuliwe viatu vya wazi (sandals) kwa ajili ya kushindia na visiwe yeboyebo. Yebo yebo vitatumika bafuni na maliwatoni pekee.
(e) Soksi jozi mbili nyeusi /khaki za shule.
(e) Mkanda mweusi.
(f) Sweta moja (01) rangi ya kijivu.
(g) Tai ya kijivu iliyoiva yenye kufanana na kitambaa cha suruali.

**2:2. VIFAA VYA MICHEZO NA SHAMBA DRESS**

(i) Suruali mbili (2) nyeusi, chini upana inchi 14. Zitavaliwa nje ya darasa.
(ii) T-shirt nyekundu mbili (2) zenye maandishi ya jina la shule. *(Zinapatikana jirani na Shule Tsh.15,000/=* kila moja, *utanunua mwenyewe).*
(iii) Track suit nyeusi kwa ajili ya mazoezi au kwa ajili ya kusomea usiku kuzuia mbu na baridi.
(iv) Pia aje na raba za michezo.
(v) Shuka mbili (2), foronya 2 (rangi ya light blue), blanket 1 na chandarua 1. (Rangi nyeupe).
(vi) Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe vyote vya bati). Vyombo vya plastiki haviruhusiwi.
(vii) Ndoo mbili za lita kumi zenye mifuniko.
(viii) Fagio moja ya chelewa, Ufagio wa kudekia (squiser) 1, na mfagio mmoja wa ndani (soft Broom) au mfagio mgumu wa chooni (hard broom).
(ix) Godoro 1 ichi 2.5 (linapatikana katika duka lililopo karibu na shule)
(x) Jembe lenye mpini kwa wanafunzi wa tahasusi ya CBG na panga moja kwa wanafunzi wa tahasusi ya HGL.

**ZINGATIA:**

***- Ni marufuku mwanafunzi kuja na simu shuleni au kuhifadhi simu kwa mwalimu. Utaratibu wa mawasiliano yoyote atapewa shuleni na ofisi ya malezi,***

***-Nguo ambazo siyo sare ya shule haziruhusiwi shuleni, ukaguzi wa vifaa vyote vinavyoingizwa shuleni utafanyika na sharti mwanafunzi aje shuleni akiwa amevaa sare ya shule.***

***- mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni aje na sanduku moja la bati (tranka) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake.***

***- Mzazi jitahidi kumnunulia mwanao mahitaji yote ili kuepusha usumbufu wa ruhusa zisizo za lazima kwenda nje ya shule.***

**(a) Michango inayotakiwa kulipwa shuleni na kila mzazi ni;-**

(i) Shilingi **65,000/=** kwa ajili ya michango ya uendeshaji wa shule.
(ii) Shilingi **5,000/=** kwa ajili ya kitambulishocha shule.
(iii) Shilingi **5,000/=** kwa ajili ya tahadhari.
(iv) Shilingi **5,000/=** kwa ajili ya nembo ya shule.
( Fedha ya tahadhari **5,000/**= (Haitarejeshwa).
**JUMLA ya michango yote Tsh. 80,000/=**

Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya shule, **Namba 50210007255** Jina la akaunti ni **A.A.KARUME HIGH SCHOOL GENERAL ACCOUNT.**

Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye ***pay in slip*** na mwanafunzi aje nayo shuleni. Shule haitahusika na malipo yanayofanywa kwa taslimu hivyo mzazi zingatia kuweka fedha kwenye akaunti na kumpatia mwanafunzi fomu ya benki. ( bank Pay in slip).

**MAHITAJI MENGINE MUHIMU:**

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-
(i) Rimu ya karatasi 2 (Kwa mwaka).
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika:

(a)Tahasusi ya **CBG** waje na vitabu vifuatavyo : -

- Modern Chemistry A,B,C -Part 1
- Modern Chemistry A, B,C- Part 2
- Physical Chemistry- by S. Chandi
- Organic Chemistry - by S. Chandi
- Conceptual Chemistry.
- Advanced Level Chemistry.
- Human and Economic Geography- by D.T. MSABILA
- Integrated Approach to Physical Geography- by D.T. MSABILA
- Practical Geography for Advanced Learners- by W.Njiku.
- Practical Geography for Advanced Level – by Z. Kamili.
- Physical Geography in Diagrams from Africa –by R.B. Bannet.
- Biological Science for Advanced Level by _ D.J.Taylor, N.P.O.Green, G.W.Stout
- Principles of Biology.
- Biology for Advanced Level Secondary School- by Tanzania Institute of Education (TIE)
- Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies, Form 5&6. By Bukagile, G.R. et.al (2010).

(iii) Dissecting Kit kwa wanafunzi wa CBG.
(iv) Scientific calculator kwa wanafunzi wa CBG

(b)Tahasusi ya **HGL** waje na vitabu vifuatavyo : -

- Essentials in Advanced History Paper 2 –by Salehe Yassin
- Contemporary Historical Events, History 1 -by Mwl. Shibital C.K.Tumaini
- Practical Geography for Advanced Learners - by W.Njiku
- Practical Geography for Advanced Level – by Z. Kamili
- Physical Geography in Diagrams from Africa –by R.B. Bannet
- Oxford Advanced Learners' Dictionary
- Advanced Level English Language – by Oxford
- Advanced Level English Language – by Nicholaus Asheli
- Contemporary Approach for Advanced Level: **General Studies**, Form 5&6. – by Bukagile, G.R. et.al (2010).

(v) kila Mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa na result slip ya kidato cha nne.

3. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i) Wizi.
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi) Kusuka nywele kwa mtindo wowote haikubaliki. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) Kufuga ndevu.
viii) Ulevi au unywaji wa pombe au matumizi ya dawa za kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara.
x) Uasherati, au uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv) Kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xvi) Kudharau bendera ya Taifa.
xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu. n.k
xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule aendapo nyumbani wakati wa likizo na wakati wa kurejea shuleni, hivyo mzazi hakikisha mwanao amevaa **SARE YA SHULE** wakati wa kuondoka na kurudi nyumbani. Kutokufanya hivyo kutamsababishia mwanafunzi adhabu.

5. Viambatisho na Fomu muhimu unazopaswa kujaza na kuleta shuleni:-
   (a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
   (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ Mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.
   (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakatolewa na shule.
   (d) Picha nne (4) za wazazi (02) za ndugu wa karibu (02) wanaoweza kuja kumtembelea mwanafunzi Pamoja na namba zao za simu.
6. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA AMANI ABEID KARUME SEKONDARI**
**MOTO WA SHULE**
**“ELIMU KWA JASHO” - EDUCATION WITH AN EFFORT**

PICHA YA
MWANAFUNZI

**HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:**

Jina kamili la Mwanafunzi: ………………………………………Umri……………..
Tarehe ya kuzaliwa: ………………Mahali alipozaliwa……………………………….
Wilaya …………………………………………………… Mkoa …………………
Shule ya Sekondari atokayo: …………………………………………………………

**MKATABA/MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………………………. Mwanafunzi wa kidato cha tano;

1. Nimesoma na kuzielewa kanuni na sheria za shule, naahidi kuwa nitazitekeleza, Kadri ya uwezo wangu.Nikishindwa kuzitekeleza, hatua zichukuliwe na Uongozi wa shule kulingana na kosa dhidi yangu.
2. Ninaahidi kwamba sitashiriki Mgomo shuleni wala kuhamasisha au kushawishi wengine kugoma kwa namna yeyote ile. Na iwapo itabainika kuwa nimehusika Hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina la Mwanafunzi ………………………………………………..
Saini ya mwanafunzi………………………………………………
Tarehe ……………………………………………………………………..

Mtendaji wa Kata ……………………………………………………..
Saini ………………………………………………………………………………
Muhuri…………………………………………………………………………
Namba ya simu………………………………………………………………
Tarehe ……………………………………………………………………………

# FOMU YA MZAZI

Mimi ……………………………………………………………….Mzazi/mlezi ninakubali mtoto wangu……………………………………… Asome katika shule ya Sekondari…………………….……………………. Tangu tarehe …………………… Hadi……………………….

(a) Ninakiri kukubaliana na kwamba nitakuwa nikilipa ada na michango yote na kufuata maelekezo yatakayotolewa na shule na kuyafanyia kazi.

(b) Naelewa ya kuwa nafasi hii ya mtoto wangu kuingia kidato cha tano (5) siyo haki yake ila ni Bahati aliyotunukiwa na Taifa. Naahidi yakuwa nitahakikisha atafuata sheria na kanuni za shule na akishindwa hatua zozote zichukuliwe dhidi yake.

Jina la Baba Mzazi/mlezi……………………………………………………
Saini ………………………………………………………………………………..
Namba ya simu ………………………………………………………………….
Tarehe ………………………………………………………………………………

PICHA

Jina la Mama Mzazi/mlezi…………………………………………………
Saini …………………………………………………………………………………..
Namba ya simu ……………………………………………………………………
Tarehe ………………………………………………………………………………

PICHA

**TAARIFA ZA NDUGU ANAYERUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI:**

1. Jina la Ndugu/Mlezi…………………………………………………….
   Saini ………………………………………………………………………..
   Uhusiano……………………………………………………………………
   Namba ya simu ………………………………………………………

PICHA

2. Jina la Ndugu/Mlezi……………………………………………………….
   Saini ……………………………………………………………………………….

   Uhusiano……………………………………………………………………………..
   Namba ya simu ……………………………………………………………

PICHA

Mwenyekiti wa Mtaa/Mtendaji
Jina ……………………………………………………………………………………..
Namba ya simu ………………………………………………………………..
Saini ……………………………………………………………………………………..
Muhuri ……………………………………………………………………………

**KONDOA DISTRICT COUNCIL**

**AMANI ABEID KARUME HIGH SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a medical officer in respect of all form five entrants:

Full name: …………………………………………………..Age ………………..
Sex…………… Year ……………………

1. Blood count (Red and White) ………………………………………………..
2. Urine analysis Test…………………………………………………………
3. Syphill Test………………………………………………………………..
4. T.B. Test …………………………………………………………………..
5. Eye Test ……………………………………………………………………
6. Ears Test ……………………………………………………………………
7. Spleen ……………………………………………………………………..
8. Abdomen ………………………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION**
E.g. Physical defects or impairment(s), infections, chronic or family diseases, etc
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

…………………………………… ………………………………………
Name and designation Signature and official Stamp

…………………………………… …………………………………….
STATION DATE

**NOTE:**
This form should be sent to school with acceptance form or brought when you come to school. No student will be enrolled without certification of physical fitness.

Medical officer during the course of this examination, please attend the individual according to any diagnosed case.